

# Mkopo

## Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako



### Mkopo ni nini?

Mkopo ni pesa unazokopa kutoka aliyekuazima. Unafaa kulipa kulingana na wakati muliyosikizana. Unahitaji kuzilipa pesa ulizokopa pamoja na faida, ada na gharama. Kama ukikosa kuzilipa pesa kwenye wakati kutakuwa na malipo zaidi.

Wakopeshaji pia wanaitwa credit providers. Wanakuwa pamoja na kwenye benki, umoja wa kusadiki, ujenzi wa jamii na kampuni za fedha zinazokopesha pesa. Wakopeshaji hutengeneza pesa kwa kukopesha pesa na kulipisha faida, ada na gharama kwa huduma hii.

### Faida, ada na gharama?

Faida ni kiasi cha pesa kinachoendelea unazolipa ilikutumia mkopo.

Ada na gharama ni bei zaidi za kukopesha pesa (mkopo). Zinaweza kugharamika mwezini au mwakani. Gharama hizi zaweza kuwa:

- ▶ ada mwezini kwa kuweka akaunti
- ▶ ada kama ukikosa kulipa kwenye wakati ulioteuliwa
- ▶ ada kama hutafanya malipo.

### Sheria ya Mkopo

Katika Australia wakopeshaji lazima wafuate sherai za mkopo. Hii hurekebishwa na Serikali ya Australia. Mtu ambaye anakopa pesa pia lazima afuate sheria.

### Aina za Mkopo

Kunazo aina tofauti za mikopo katika Australia na aina ya mkopo unaotumia inategemea sababu ya kukopa pesa. Mifano zingine ni kadi za mkopo, mikopo ya gari, mikopo ya nyumba, kadi za duka, mikopo ya muda mfupi na kukodisha kwa wateja.

### Kumbuka

- ▶ Mkopo ni pesa ambazo umekopa na lazima ulipe.
- ▶ Mkopo unagharama zaidi.
- ▶ Kukopa zaidi kunaweza kusababisha shida za pesa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu mkopo, tembelea tuvuti ya MoneySmart, [www.moneysmart.gov.au](http://www.moneysmart.gov.au), au upige 1300 300 630. Waweza pia kkupigia Afisa wa Huduma ya Maelezo ya Kifedha kwenye 13 23 00 ambaye atakusaidia kuongoza mkopo wako.

Kufanya utaratibu kwa faili ya mkopo, tembelea [www.mycreditfile.com.au](http://www.mycreditfile.com.au).

### Hussein anapata mkopo wa gari

Hussein anataka kununua gari ya pili. Anataka gharama ya uandikishaji na bima (karibia \$1,000) iwekwe na ameamua kutumia hadi \$5,000. Hii inamaanisha kuwa bei ya gari haiwezi zidi \$4,000. Hana akiba kwa hivyo lazima akope pesa.

Jumamosi moja Asubuhi, Hussein alienda kwenye yadi ya kuuza magari zilizotumiwa ili kutafuta gari liliyotumiwa. Yeye aliona moja analolipenda kwa \$3,900. Hussein anampata muuzaji gari na kumuuliza maswali mengine kuhusu gari. Hussein anataka kujua kama gari ile ni ya kutegemewa, mwaka ngani ilitengenezwa na kama ni salama kuiendesha. Hussein anaamua kuwa angependelea kununua gari. Mtu anayehusika na fedha kwenye yadi ya gari anasema kuwa Hussein anaweza kuomba mkopo lakini lazima ajibu maswali kwanza.

Hussein anampa maelezo mtu anayehusika na fedha maelezo. Mtu anayehusika na fedha anamwambia Hussein kuwa anaweza kupata mkopo wa \$4,900 (ambao pia atalipia kujiandikisha na bima).

Mtu anayehusika na fedha alimpatia Hussein mkataba wa mkopo na kumuuliza yeye kusoma na kutia sahihi. Hata hivyo rafiki wa Hussein alimwambia kuwa 'Usifanye kutia sahihi kitu ambacho huelewi.' Hussein anataka kusoma mkataba wote ili aulize kama anaweza kupeleka nyumbani kusoma kwanza.' Alikubaliwa kukutana tena na mtu anayehusika na fedha siku ya Jumatatu asubuhi.

Hussein aliusoma mkataba wa mkopo na kurundi tena kwenye yadi ya gari pale Jumatatu ili kukutana na mtu anayehusika na fedha. Baada ya kusoma mkataba wa mkopo, Hussein ana maswali mengi. Anauliza mtu anayehusika na fedha nini itakuwa taslimu kiasi cha mkopo, ada itakuwa vipi, kiasi ngani na mara ngapi atahitaji kufanya malipo, na mkataba wa mkopo utakuwa wa urefu ngani. Hussein alielewa kabisa muda na masharti ya mkopo na kutia ahihi mkataba na kununua gari.

This page has been intentionally left blank.